**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.** AB.392/512/01/1224 **Tarehe:** 20/11/2025

Makatibu Wakuu wa Wizara,
Wakurugenzi Wakuu wa Mashirika ya Umma,
Wakuu wa Idara Zinazojitegemea,
Watendaji Wakuu wa Mamlaka/Wakala za Serikali,
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Majiji, Miji na Wilaya,
Wakurugenzi wa Taasisi na Mashirika Binafsi,
**TANZANIA.**

Ndugu,

**YAH: MWALIKO WA KONGAMANO LA 16 LA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Bodi inafuraha kukutaarifu kuwa itakuwa mwenyeji wa Kongamano la 16 la Mwaka la Ununuzi na Ugavi **tarehe 19 hadi 21 Desemba, 2025 AICC Arusha.** Kongamano hili huwaleta pamoja wadau wote wa shughuli za za ununuzi na ugavi kutoka ndani na nje ya nchi ili kujadili na kubadilishana uzoefu katika masuala ya kitaalamu katika sekta ya na sekta binafsi kwa kuzingatia kaulimbiu isemayo; Mabadiliko ya kidijitali ni muhimu katika kuboresha usimamizi wa mnyororo wa ununuzi na ugavi kuelekea maendeleo endelevu "(

3. Hivyo, Bodi inakuomba ukiwa kama mwajiri na mdau muhimu wa PSPTB kitaaluma kuwafadhili wataalam wako wa ununuzi na ugavi, wajumbe wa bodi ya zabuni na watumishi wa idara tumizi kutoka fani mbalimbali pamoja na watoa maamuzi wengine wanaohusika katika shughuli za ununuzi na ugavi ili waweze kuhudhuria kongamano hili muhimu. Kongamano hili litawasaidia kubadilishana uzoefu, maarifa na ujuzi mahsusi kwenye mnyororo mzima wa ununuzi na ugavi katika zama hizi za kidigitali. Ni matarajio ya PSPTB kuwa kupitia Kongamano hili washiriki wataweza kuboresha utendaji kazi wao binafsi na taasisi zao ili kuleta tija

*Mkandarasi Place (Ghorofa ya saba), S.L.P. 2663, Dodoma. Simu: +255 22 2865860*
*Nukushi: +255 22 2862138. Tovuti: http://www.psptb.go.tz. Barua pepe: info@psptb.go.tz*

katika maendeleo ya sekta binafsi na sekta ya umma. Pia, washiriki waliosajiliwa na PSPTB wataidhinishiwa **saa 24** za maendeleo ya kitaaluma (*CPD hrs*) kama hitaji lao la msingi kitaaluma.

4. Kwa wataalamu wote, usajili wa ushiriki ufanyike mtandaoni kupitia akaunti zao za usajili mtandaoni. Washiriki wasio na usajili wa PSPTB, usajili wa ushiriki wao utafanyika mtandaoni kupitia; https://registration.psptb.go.tz/ kwenye tangazo la kongamano hili. Ada za ushiriki zimefafanuliwa katika jedwali hapa chini:

| Washiriki | Ada ya ushiriki |
|---|---|
| Wataalam waliosajiliwa na PSPTB | TZS. 600,000/= |
| Washiriki wengine | TZS. 750,000/= |
| Wanafunzi wasio na ajira | TZS. 350,000/= |
| Washiriki kutoka nje ya Tanzania | TZS. 1,000,000/= |
| Washiriki kwa njia ya Mtandao | TZS. 400,000/= |

5. Ada hizi za ushiriki ni kwa ajili ya maandalizi na uwasilishwaji wa mada, nyenzo za kongamano, kifungua kinywa na chakula cha mchana tu.

6. Tunakushukuru kwa ushirikiano wako katika kujali taaluma hii adhimu ya ununuzi na ugavi kwa maendeleo ya Taifa.

**NB:** Tafadhali, kumbuka kuwa hakuna washiriki watakaoruhusiwa kuhudhuria mkutano wa kongamano hili bila kukamilisha malipo ya ada za ushiriki zilizotajwa hapo juu. Mwisho wa kulipa ada ya ushiriki ni tarehe **30 Novemba, 2025**.

7. Wasalaam,

Digitally Signed By Godfred B. Mbanyi
Thu Nov 20 12:12:03 EAT 2025

Godfred B. Mbanyi
**MKURUGENZI MTENDAJI**

*GBM/pgm.*

*Mkandarasi Place (Ghorofa ya saba), S.L.P. 2663, Dodoma. Simu: +255 22 2865860*
*Nukushi: +255 22 2862138. Tovuti: http://www.psptb.go.tz. Barua pepe: info@psptb.go.tz*